WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 62 | Jan 1 - 30 2025



# DKT. BITEKO AAGIZA KITUO CHA HUDUMA KWA WATEJA TANESCO KUSUKWA UPYA

WIZARA YA NISHATI +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**

Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika

**WAPIGA PICHA**

Amanzi Kimonjo
Henry Kilasila
Mustafa Shahame
Isaya Mwakajana


**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga

© NISHATI 2024

# DKT. BITEKO AAGIZA KITUO CHA HUDUMA KWA WATEJA TANESCO KUSUKWA UPYA

- Akerwa na kusuasua kwa utendaji wa Kituo hicho
- Awataka watendaji kuondokana na kufanya kazi kwa mazoea
- Ahoji sababu za kutelekezwa kwa maelekezo yake ya 2024



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, akizungumza mara baada ya kutembelea Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Shirika la Umeme Nchini, (TANESCO) na kufuatilia utekelezaji wa maelekezo yake aliyoyatoa mwezi Aprili, 2024.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameagiza kufumuliwa kwa Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Shirika la Umeme Nchini, (TANESCO) kufuatia kituo hicho kushindwa kuwahudumia Wananchi kwa viwango vinavyotarajiwa.

Ametoa agizo hilo leo tarehe 9 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam baada ya kutembelea kituo hicho pamoja na mambo mengine kufuatilia utekelezaji wa maelekezo yake aliyoyatoa mwezi Aprili, 2024.

Dkt. Biteko ameshangazwa na hatua ya TANESCO kuweka kando maelekezo ya mwezi Aprili 2024 yaliyolitaka Shirika hilo kuondokana na matumizi ya namba za kulipia kwenye utoaji wa huduma na kuomba namba ya bure ya huduma (free toll number) kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania -TCRA ili kuwapa unafuu wananchi wanaohitaji huduma za TANESCO.

“ Wewe ulishapiga simu, pesa yako ikakatwa na huduma usiipate? Wananchi wanaumia sana!” naagiza kuundwa upya kituo ili kuongeza ufanisi na tija kwa Wananchi, “kituo hiki kinategemewa na Watanzania wengi na huduma inayotolewa hapa hairidhishi kabisa,” amesema Dkt. Biteko.

Ameongeza kuwa, Serikali ya Rais Samia imetoa fedha nyingi kuhudumia kituo hicho lakini utendaji wake ni mbovu kuliko huduma ya kituo.


TANESCO ilielekezwa kuachana na matumizi ya namba za kulipia Kwenye utoaji wa huduma na kuomba namba ya bure ya huduma (toll number) kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA ili kuwapa unafuu wa Wananchi wanapopiga kuhitaji huduma za TANESCO.

Dkt. Biteko ametoa wiki moja kwa uongozi wa TANESCO kufanya maboresho ya Kituo hicho na matokeo yake yawe wazi kwa Wananchi kutokana na huduma zake.

Akizungumzia utendaji wa Kituo hicho, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Mha. Abubakar Issa amesema kulikuwa na changamoto za kibajeti. Aidha amesema kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania TCRA watakaa haraka na kuanza matumizi ya namba bila malipo ili kutoa unafuu kwa wananchi na kuleta tija kwa watumiaji.

# TANZANIA IPO TAYARI KUPOKEA WAKUU WA NCHI AFRIKA KATIKA MKUTANO WA NISHATI WA MISSION 300 -DKT.KAZUNGU

- Aliambia Jukwaa la IRENA UAE kuwa Tanzania imejipanga vema kwa ujio huo.
- Asema Tanzania imerekehisha sheria ya uwekezaji kuruhusu sekta binafsi kutekeleza miradi
- Nchi wanachama IRENA wataka wabia wa maendeleo kuwekeza kwenye miradi ya nishati ambayo ni rafiki kwa mazingira




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati anayeshughulikia Umeme na Nishati Jadidifu Dkt Khatibu Kazungu,(katikati) akiwa kwenye mkutano wa Baraza la 15 la wakala wa kimataifa wa nishati jadidifu (IRENA).

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati anayeshughulikia umeme na nishati jadidifu Dkt Khatibu Kazungu amesema ,Tanzania imejipanga vema kupokea ugeni wa Wakuu wa Nchi 53 wa Afrika watakaohudhuria mkutao wa wakuu wa nchi wa masuala ya nishati unaotarajiwa kufanyika tarehe 27 hadi 28 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.

Dkt Kazungu ameyasema hayo kwenye mkutano wa Baraza la 15 la wakala wa kimataifa wa nishati jadidifu (IRENA) wakati akiwasilisha mada kwenye mjadala wa ngazi ya juu wa Mawaziri wenye lengo la kujadili namna ambavyo nchi wanachama wanaweza kutumia fursa ya ushawishi kwa wadau wa maendeleo kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya nishati jadidifu ambayo ni rafiki kwa mazingira

‘‘ Nipende kuwajulisha kuwa Tanzania ni mwenyeji wa mkutano huo wa masuala ya nishati na ajenda hii kama nchi tumeibeba kwa vitendo kuhakikisha waafrika Milioni 300 kusini mwa jangwa la Sahara wanapata umeme ifikapo mwaka 2030 na natoa rai kwa nchi wanachama wa IRENA kuibeba ajenda hii kwa vitendo.’’ Amesema Dkt. Kazungu

Amesema mkutano wa M300 utaangazia pia mageuzi kwenye sekta ya nishati na kuangalia uwezekano wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuunganisha wateja sambamba na ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye utekelezaji wa miradi ya pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia

Aidha Dkt. Kazungu amewaambia wajumbe wa IRENA kuwa kauli mbiu itakayoongoza mkutano huo ni kuharakisha upatikanaji wa

# WIZARA YA NISHATI YAPOKEA MAGARI KUTOKA MRADI WA UMEME WA NYAKANAZI



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Bi Ziana Mlawa (kushoto wa kwanza) akiongoza watumishi mbalimbali kupokea magari sita kutoka Mradi wa Usafirishaji wa Umeme Nyakanazi katika Ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma Januari 09, 2025.

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Bi Ziana Mlawa ameongoza Watendaji mbalimbali kupokea magari sita kutoka Mradi wa Usafirishaji wa Umeme Nyakanazi katika Ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma Januari 09, 2025.

Katika magari hayo sita yaliyopokelewa, moja litaenda Wizara ya Fedha, mawili yataenda Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na magari matatu yatabaki Wizara ya Nishati.

nishati Afrika ili kuwatoa gizani waafrika wapatao milioni 685 kati ya Bilioni 1 ambao hawana nishati ya umeme

Dkt Kazungu amesisitiza kuwa Serikali imefanya marekebisho ya sheria ya uwekezaji ili kutoa fursa kwa sekta binafsi kushirikiana na Serikali kutekeleza miradi ya nishati jadidifu kutokana na umuhimu wake

Amesema Tanzania inawashukuru sana wabia wa maendeleo kwenye utekelezaji wa miradi ya nishati jadidifu kama vile Benki ya Dunia, Benki ya maendeleo ya Afrika AfDB, AFD, KFW kwa kufadhili miradi mbalimbali ya nishati jadidifu nchini ikiwemo ule wa Kakono na Malagarasi ambayo iko kwenye hatua za utekelezaji

Kwa upande Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Nishati na Mabadiliko ya Tabia Nchi kutoka Benki ya AfDB, ambao pia wanafadhili miradi ya nishati jadidiifu kwa upande wa Afrika Kevin Kariuki alisema kuwa utashi wa kisiasa, uainishaji wa sera za wazi vinahitajika sana kwenye utekelezaji wa miradi ya umeme kwa nchi za Afrika ili iweze kuleta tija kwa wananchi wake

Alisema ni wakati sasa kwa nchi za Afrika kuchangamkia fursa za utekelezaji wa miradi ya nishati ambayo ni rafiki kwa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza hewa ya ukaa na kuzitaka jumuiya za kimataifa kuunga mkono azimio hilo kwa vitendo.

# WIZARA YA NISATI YAWASILISHA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2024/2025 KATIKA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI

- Maeneo ya kipaumbele yaliyotekelezwa kwa mwaka 2024/2025 yaelezwa
- Ni pamoja na hali ya uzalishaji na upatikanaji wa Nishati ya Umeme nchini



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga, akizungumza wakati wa kuwasilisha taarifa utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2024/2025 katika Kipindi Cha Julai hadi Desemba 2024 katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini

Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga (Mb) ameongoza Menejimenti ya Wizara ya Nishati kuwasilisha taarifa utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2024/2025 katika Kipindi Cha Julai hadi Desemba 2024 katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Taarifa hiyo imewasilishwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Nishati Petro Lyatu ambaye ameeleza kuwa Wizara ya Nishati imetekeleza bajeti katika maeneo mbalimbali ikiwa ni yale ya kipaumbele na kimkakati pamoja na kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji ,usafirishaji na usambazaji wa Umeme Ili kuufikisha gridi ya Taifa katika mikoa iliyosalia.

Amesema Wizara imeendelea kupeleka nishati Vijijini ikiwemo kusambaza umeme katika vitongoji Tanzania Bara pamoja na kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia ikiwa ni sambamba na mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika.

Amesema Wizara ya Nishati inaendelea kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa umeme wa uhakika na unaokidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa na kuongezeka kufikia Megawati 3,091.71 mwezi Desemba,2024.

Amesema ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali hususani Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ambapo hadi Desemba 2024 mitambo mitano (5) kati ya tisa ilikuwa imekamilika na inazalisha umeme na kuingizwa katika Gridi ya Taifa.

Vile vile, Lyatu amebainisha kuwa Wizara imekamilisha Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati (2024/2025) mwezi Novemba 2024 ambao ulizinduliwa Desemba 3, 2024 wakati wa Kongamano la Kikanda katika Nchi za Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) la Matumizi Bora ya Nishati, Mkakati ambao pamoja na masuala mengine unalenga kuendelea kuhakikisha Watanzania kutumia Nishati kwa ufanisi Ili kupunguza gharama za Matumizi pamoja na kuendelea kuimarisha upatikanaji na Matumizi ya Nishati safi ya Kupikia.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Dk. David Mathayo David baada ya kupokea taarifa amesema kuwa "Wizara Haina budi kuendelea kuunga mkono Sera ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan juu ya Matumizi ya Nishati safi ya Kupikia kwa Watanzania,kwa kuendelea kufanya tafiti, kuhamasisha watumiaji, kutoa elimu na kuanzisha sheria ya kulinda miundombinu mbalimbali ya nishati ya kupikia na kuhakikisha gesi kwa watumiaji inapatikana kila Kona ya Tanzania".

# UWEZO WA MITAMBO YA KUFUA UMEME WAFIKIA MEGAWATI 3,091.71- MHE.KAPINGA

- Wateja wapya 109,918 waunganishiwa na huduma ya umeme nchini
- Kamati ya Bunge yaipongeza TANESCO kwa kuimarisha Miundombinu ya umeme



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga, akizungumza wakati wa kujadili taarifa ya Wizara ya Nishati kuhusu hali ya uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini kwa kipindi cha kuanzia mwezi Septemba hadi desemba, 2024 kwa wajumbe wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) limesema kuwa uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa hadi kufikia mwezi Desemba, mwakajana ni jumla ya Megawati 3,091.71 ikilinganishwa na Megawati 2,842.96 zilizokuwepo mwezi septemba, 2024 ikiwa ni ongezeko la Megawati 248.75 sawa na asilimia 8.75.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga Januari 16, 2024 jijini Dodoma, wakati wa kujadili taarifa ya Wizara ya Nishati kuhusu hali ya uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini kwa kipindi cha kuanzia mwezi Septemba hadi desemba, 2024 kwa wajumbe wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

"Ongezeko hilo lilitokana na kuingia kwa Megawati 235 kutoka katika Mradi wa JNHPP pamoja na mitambo ya Kigoma kuingia kwenye Gridi ya Taifa." Smesema Mhe. Judith Kapinga

Ameeleza kuwa, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) katika hatua nyingine limeendelea na ukarabati mitambo mbalimbali ya kuzalisha umeme ikiwemo ile ya Kihansi, Kidatu pamoja na Ubungo ili kuwezesha Taifa kuwa na umeme wa uhakika muda wote.

Aidha, Kapinga amesema kuwa hali ya miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini inaendelea kuwa nzuri jambo ambalo limechangia upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa wateja na miundombinu hiyo inayojumuisha njia za kusafirisha umeme zenye jumla ya urefu wa kilomita 8, 025.38 pamoja na njia za kusambaza umeme zenye urefu wa kilomita 197, 597.34.

Kupitia miundombinu hiyo, Shirika limeweza kuunganisha wateja wapya 109,918 ndani ya kipindi cha kuanzia mwezi Septemba, 2024 hadi mwezi Desemba, 2024. Ongezeko la wateja hao limewezesha jumla ya wateja waliounganishiwa umeme nchini kufikia 5, 225, 193.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. David Mathayo David ameipongeza Wizara kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kuendelea kuimarisha miumbombinu mbalimbali ya uzalishaji, usambazaji na usafirishaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

# DKT. BITEKO AKAGUA UJENZI WA OFISI YA WAZIRI MKUU NA JENGO LA OFISI YA NISHATI MJI WA SERIKALI-MTUMBA

- Aagiza ujenzi ukamilishwe haraka
- Majengo yakamilika kwa asilimia 88
- Wakandarasi waomba nyongeza  siku 90



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko,akizungumza mara baada ya kukagua na kupata maelezo ya wataalam na wasimamizi wa majengo mbalimbali ya Wizara na kuagiza majengo hayo yakamilishwe kabla ya mwezi Aprili, 2025.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amefanya ziara katika Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma kukagua maendeleo ya ujenzi majengo ya Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu pamoja na Wizara ya Nishati ambayo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 88.

Akizungumza baada ya kukagua na kupata maelezo ya wataalam na wasimamizi wa majengo hayo, Naibu Waziri Mkuu Biteko amewapongeza wakandarasi kwa hatua iliyofikiwa na kuagiza majengo yakamilishwe kabla ya mwezi Aprili, 2025.

“Serikali chini ya Rais Samia imefanya kazi kubwa, tayari imetoa zaidi ya asilimia 90 ya malipo kwa wakandarasi kwa maana ya kwamba ni kiasi kikubwa zaidi ya ukamilifu wa jengo, Najua SUMA JKT mkifanya kazi kwa operesheni mnaweza kukamilisha ujenzi wa jengo hili hata kabla ya muda uliopangwa” amesema Dkt. Biteko

Msimamizi wa Ujenzi Jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, kutoka SUMA JKT Kanali Mbaraka Magogo ameomba Serikali iwaongezee muda wa miezi mitatu kuanzia sasa ili kukamilisha ujenzi na majengo yatumike ifikapo mwezi Aprili, 2025.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ametembelea jengo la Wizara ya Nishati ambapo amemtaka mkandarasi ambaye ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuharakisha ukamilishaji ujenzi wa jengo hilo na lianze kutumika kabla ya mwezi Aprili, mmwaka huu.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu, Mhe. Ummy Nderiananga amemshukuru Naibu Waziri Mkuu kwa maelekezo yake na kusema Ofisi itaendelea kusimamia kwa karibu ili kuhakikisha kwamba malengo yanafikiwa kama ilivyopangwa.

“Kwa niaba ya Waziri Nchi Mhe. Lukuvi (William Lukuvi) namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa ziara hii ambayo ni chagizo kwetu kuhakikisha kwamba ujenzi wa majengo haya unakamilika kwa wakati kama walivyoomba wakandarasi, kwa kuwa sisi ni waratibu inabidi tuwe mfano kwa wengine.” Amesema Mhe. Ummy.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felichesmi Mramba amemhakikishia Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kuwa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Wizara hiyo ziko katika hatua nzuri na amekuwa akiwasiliana na HAZINA kwa ajili ya upatikanaji wake.

“Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, tuko katika hatua nzuri hata leo asubuhi nimezungumza na PST (Katibu Mkuu Wizara ya Fedha) na nimehakikishiwa kwamba fedha hizo zitapatikana,” amesema Katibu Mkuu Mramba.

# DIPLOMASIA YA RAIS SAMIA INAWALETA WAKUU WA NCHI AFRIKA KUSHIRIKI MKUTANO WA M300 -DKT. BITEKO

- Asema mafanikio ya Sekta ya Nishati nayo yameibeba Tanzania Mkutano wa M300
- Vijiji vyote Tanzania vyafikishiwa umeme
- Ataja faida za Mkutano wa M300 nchini



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akifanya mahojiano kupitia kipindi cha Jambo Tanzania kinachorushwa na Kituo cha Utangazaji TBC 1 Januari 10, 2024 (Picha na Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati)

Imeelezwa kuwa Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ujulikanao kama Mission 300 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo diplomasia ya kiuchumi chini ya uongozi wa Rais, Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan

Hayo yamesemwa tarehe 10 Januari 2025 na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt. Doto Biteko wakati akizungumzia Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika utakaofanyika tarehe 27 na 28 Januari 2025 jijini Dar es Salaam.

"Rais, Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania kimataifa, hii imepeleka taasisi za kimataifa, kampuni na wawekezaji kuona Tanzania kuwa ni sehemu sahihi ya kufanya biashara na uwekezaji na mfano halisi ni Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo Afrika kuichagua Tanzania kufanya mkutano huu mkubwa wa kimataifa utakahudhuriwa viongozi kitoka nchi 54 barani Afrika." Amesema Dkt. Biteko

Ameongeza kuwa, sababu nyingine kubwa ya Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano huo ni mafanikio yaliyofikiwa katika sekta ya nishati ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme kwa wananchi suala linaloendana na Ajenda ya mkutano huo ya kuharakisha kupeleka umeme kwa wananchi milioni 300 barani Afrika ifikapo 2030 kati ya watu milioni 685 ambao bado hawana umeme.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (kulia) pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa (kushoto) wakiingia katika Studio za TBC 1 kufanya mahojiano kuhusu Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika. (Picha na Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati)

"Taifa limepiga hatua kubwa katika Sekta ya Nishati, tunamshukuru Mhe. Rais kwa msukumo mkubwa anaotoa katika Sekta ya Nishati, taifa lina umeme wa kutosha na wa ziada, uzalishaji sasa umepanda kutoka megawati 1470 hadi megawati takriban 3,077." Amesema Dkt.Biteko

Amesema upatikanaji wa umeme barani Afrika kwa sehemu kubwa uko chini ya asilimia 50 lakini Tanzania imepiga hatua kubwa na ipo kwenye asilimia zaidi ya 78.

Akiongeza kuhusu mafanikio ya Sekta ya Nishati, Dkt.Biteko amesema vijiji vyote 12,318 Tanzania sasa vimesambaziwa umeme na tathmini iliyofanywa na Benki ya Dunia barani Afrika mwaka jana imeonesha kuwa Tanzania iliongoza kwa kusambazia wananchi umeme vijijini .

Dkt. Biteko ameeleza kuwa, baada ya umeme kufika kwenye vijiji vyote sasa kasi inaelekea kwenye vitongoji ambapo katika vitongoji 64,000 nchini, vitongoji takriban 36,000 vimepelekewa umeme.

Ametaja faida za mkutano wa M300 kwa Tanzania kuwa ni pamoja na kuongeza fursa za kupata fedha za kuendelea miradi mbalimbali, kuongeza fursa za uwekezaji, kupata uzoefu kutoka kwa waliofanikiwa zaidi kwenye sekta ya nishati na kuongeza heshima ya nchi kimataifa.

Ameongeza kuwa faida nyingine ni kuharakisha upatikanaji umeme nchini ambapo kiasi cha wananchi watakaounganishiwa umeme kupitia M300 ni milioni 8.3 ifikapo 2030 na hivyo kuifanya Tanzania kuunganisha wateja milioni 13.5 kufikia 2030 Kutoka milioni 5.2 ya sasa.

# PICHA MBALIMBALI ZA VIONGOZI WALIOSHIRIKI MKUTANO WA NISHATI WA NCHI ZA AFRIKA KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JULIUS NYERERE (JNICC)

















AFRICA ENERGY SUMMIT
MISSION 300
AFRICA ENERGY SUMMIT